# SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

## WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

## MUHTASARI WA SANAA NA UFUNDI
## KWA ELIMU YA MAANDALIZI ZANZIBAR

TAASISI YA ELIMU ZANZIBAR

2012

© Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, 2012

Haki zote zimehifadhiwa, hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa, maandishi nukta nundu na kutoa Muhtasari huu kwa jinsi yoyote ile bila ya idhini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Umetayarishwa na:
Taasisi ya Elimu Zanzibar
S.L.P. 840
**Zanzibar**

# YALIYOMO

Ukurasa

YALIYOMO ........ ii
Utangulizi: ........ iii
Ujuzi wa Jumla wa Somo la Sanaa na Ufundi ........ iii
Malengo ya Jumla ya Somo la Sanaa na Ufundi ........ iv
MUHTASARI WA MWAKA WA KWANZA ........ 1
MWAKA WA PILI ........ 10

**SANAA NA UFUNDI**

## Utangulizi:

Uwezo wa kufahamu dunia na yaliyomo unakuja hatua kwa hatua, katika miaka ya awali mtoto anakuwa na uwezo wa kutambua sauti, harufu na ladha ya vitu vilivyomzunguka.

Uwezo wa mtoto wa kubuni na kuunda unakuja kwa kuigiza mambo na baadae kuchora picha, kuzifananisha na kuzitofautisha kutokana na hali halisi ilivyo, akishaweza kujenga ufahamu katika akili yake ataweza kufikiria mambo yaliyopita, ya sasa na yajayo hatimaye kuwa mbunifu.

Sanaa na ufundi ni njia rahisi ya mtoto kuelezea fikra, hisia na matarajio yake.

Mtoto anahitaji kuongozwa na kupatiwa vifaa vitakavyoamsha ari yake ya kisanii. Mtoto apatiwe fursa ya kufanya kazi ya sanaa akiwa peke yake na katika vikundi vidogo vidogo ili asaidiane na wenzake kukuza ujuzi na mawazo yake kupitia sanaa.

## Ujuzi wa Jumla wa Somo la Sanaa na Ufundi

Baada ya kusoma somo la Sanaa na Ufundi katika skuli za Maandalizi, watoto wataonesha ujuzi wa:-

1. Kutumia milango mitano ya fahamu kwa kuhusisha vitu na uhalisi wake.
2. Kuigiza sauti na kutoa hisia mbali mbali.
3. Kuigiza michezo rahisi inayohusu mazingira yao na kuiga vitendo vinavyofanywa nyumbani.
4. Kuhusisha sauti na zana za sauti, kutofautisha aina za sauti, kuimba nyimbo na kusoma kasida.
5. Kuchora vitu mbali mbali vyenye rangi tofauti kutokana na hisia zao.
6. Kubuni na kutengeneza vitu tofauti kutokana na vitu halisi vilivyomo kwenye mazingira yao na kuviwasilisha kwa wengine.

7. Kusoma, kusimulia na kutunga hadithi fupi.

## Malengo ya Jumla ya Somo la Sanaa na Ufundi

Somo la Sanaa na Ufundi linafundishwa katika skuli za Maandalizi ili watoto waweze:

1. Kutambua matumizi ya milango mitano ya fahamu kwa kuhusisha vitu na uhalisia wake.
2. Kutambua sauti zinazotoa hisia mbali mbali.
3. Kupata stadi za ukuzaji wa vipaji vya uigizaji wa michezo rahisi inayohusu mazingira yao.
4. Kutambua zana na aina za sauti.
5. Kuzitambua nyimbo na kasida.
6. Kukuza kipaji cha uchoraji wa picha pamoja na uelezeaji hisia zao.
7. Kukuza ubunifu wa vitu kutokana na vitu halisi vilivyomo katika mazingira yao na kuviwasilisha kwa wengine.
8. Kufurahia kusoma pamoja na kupata stadi za usimuliaji na utungaji wa hadithi fupi fupi, vitendawili na vizunguka ulimi.

# MUHTASARI WA MWAKA WA KWANZA

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| 1. HISIA<br>(a) Kuona | Mtoto aweze<br>(i) Kutaja majina ya vitu mbali mbali | Kwa kutumia mbinu ya masuali na majibu, mwalimu awaongoze watoto kutaja majina ya vitu mbali mbali vilivyo ndani na nje ya darasa. | Vifaa mfano penseli, meza, viti, mawe na mchanga. | 2 |
| | (ii) Kuainisha sifa za vitu | Kwa kutumia mbinu ya chemsha bongo, mwalimu awaongoze watoto kuainisha vitu kutokana na sifa zake mfano rangi, umbo n.k | Vifaa mfano penseli, meza, viti, mawe na mchanga. | |
| (b) Kugusa | Mtoto aweze<br>(i) Kulinganisha vitu vyenye maumbo na hali mbali mbali. | Kwa kutumia mbinu ya masuala na majibu, mwalimu awaongoze watoto kutofautisha vitu vigumu, laini, vimoto, baridi. | 1. Msasa.<br>2. Vibao.<br>3. Sponji<br>4. Maji moto/maji baridi. | 2 |
| (c) Kunusa | Mtoto aweze:-<br>(i) Kuainisha harufu za vitu mbali mbali | Kwa kutumia mbinu ya onesho, mwalimu awaongoze watoto kuainisha harufu za vitu walivyovinusa. | 1. Mafuta mazuri.<br>2. Mafuta ya taa | 2 |
| | | | 3. Maua | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | | 4. Matunda | |
| | (ii) Kutofautisha harufu za vitu mbali mbali. | Kwa kutumia mbinu ya michezo (games), mwalimu awaongoze watoto kugundua tofauti za harufu za vitu. | 1. Mafuta mazuri.<br>2. Mafuta ya taa<br>.3. Maua<br>4. Matunda | |
| (d) Kuonja | Mtoto aweze:-<br>Kutaja ladha za vitu mbali mbali. | Kwa kutumia mbinu ya masuali na majibu, mwalimu awaongoze watoto kula na kunywa vitu mbali mbali ili wagunduwe na kutaja ladha mfano juisi, buni, ndimu n.k | 1. Buni.<br>2. Matunda.<br>3. Vinywaji | 2 |
| (e) Kusikia | Mtoto aweze:-<br>(i) Kuainisha sauti za vitu mbali mbali. | Kwa kutumia mbinu ya vikundi, mwalimu awaongoze watoto kuainisha milio/ sauti ya vitu walizosikiliza. | 1. Cherewa.<br>2. Wanyama.<br>3. Ngoma.<br>4. Ndeege | 3 |
| | (ii) Kuigiza sauti/milio aliousikia. | Kwa kutumia mbinu ya vikundi,mwalimu awaongoze watoto kuigiza sauti/milio ya vitu mbali mbali. | 1. Cherewa.<br>2. Wanyama.<br>3. Ngoma | |
| 2. MAINGIZO<br>(a) Sauti | Mtoto aweze:-<br>(i) Kuigiza sauti/milio ya aina mbali mbali | Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi, mwalimu awaongoze watoto kuigiza milio/sauti wanazozifahamu (Wanyama, vyombo ya moto n.k) | 1. Picha za wanayama mbali mbali<br>2. Picha za gari, | 2 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | | pikipiki n.k | |
| | (ii) Kuagua majina ya vitu vinavyotoa sauti/milio waliyoigiza | 1. Kwa kutumia mbinu ya masuali na majibu, mwalimu awaongoze watoto kuagua sauti/milio iliyoigizwa.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya nyimbo mwalimu awaongoze watoto kuimba wimbo wa uaguzi wa sauti. | 1. Pikipiki<br>2. Milio ya wanyama<br>3. Honi za gari<br>4. Chati mguso | |
| (b) Miendo | Mtoto aweze:-<br>(i) Kuigiza miendo mbaali mbali | Kwa kutumia mbinu ya igizo mwalimu awaongoze watoto kuigiza miendo mbali mbali mfano mwendo wa paka, sungura, bata n.k. | 1. Picha za wanyama na ndege.<br>2. CD | 3 |
| | (ii) Kutofautisha miendo mbali mbali | Kwa kutumia mbinu ya uchunguzi, mwalimu awaongoze watoto kutofautisha miendombali mballi. | 1. Picha za wanyama na. ndege<br>2. Chati mguso | |
| (c) Michezo | Mtoto aweze<br>Kuigiza michezo inayohusiana na mazingira yao | Kwa kutumia mbinu ya igizo, mwalimu awaongoze watoto kujipanga kwa utashi wao kwa ajili ya kuigiza michezo inayotokana na maisha ya kila siku. | 1. Vifaa halisi.<br>2. Vifaa bandia | 4 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| 3. UIMBAJI<br>(a) Nyimbo | Mtoto aweze:-<br>(i) Kuimba nyimbo mbali mbali za kielimu zenye mafunzo mazuri | Kwa kutumia mbinu burudiko (nyimbo) mwalimu awaongoze watoto kuimba nyimbo zenye maadili mema | 1. Kanda za nyimbo<br>2. CD.<br>3. Radio.<br>4. Ala za muziki | 2 |
| | (ii) Kuimba wimbo wa Taifa | Kwa kutumia mbinu burudiko, (nyimbo) mwalimu awaongoze watoto kuimba wimbo wa Taifa. | 1. Kanda za nyimbo<br>2. CD. | |
| | | | 3. Radio.<br>4. Ala za muziki | |
| (b) Kasida | Mtoto aweze:-<br>(i) Kusoma kasida ndogo ndogo. | Kwa kutumia mbinu ya kasida, mwalimu awaongoze watoto kusoma kasida | 2. CD.<br>3. Kanda za radio. | 3 |
| | (ii) Kutofautisha baina ya nyimbo na kasida | Kwa kutumia mbinu ya uchunguzi, mwalimu awaongoze watoto kuchunguza tofauti iliyopo kati ya kasida na nyimbo kwa kupitia uimbaji wa baadhi ya wanafunzi na kusikiliza kanda. | 1. Kanda za redio<br>2. CD | |
| 4. UCHORAJI<br>(a) Rangi | Mtoto aweze:-<br>(i) Kutaja majina ya | Kwa kutumia mbinu ya nyimbo, mwalimu awaongoze watoto kutaja majina ya rangi. | Rangi | 6 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | rangi | | | |
| | (ii) Kuonesha rangi mbali mbali | Kwa kutumia mbinu ya kuchambua na kupanga, mwalimu kwa kushirikiana na watoto watapembua vitu vyenye rangi zilizofanana. | 1. Kadi za rangi<br>2. Vitu yya rangi tofauti. | |
| | (iii) Kupaka rangi. | Kwa kutumia mbinu ya kumechisha, mwalimu awaongoze watoto kupaka rangi picha kwa kulinganisha. | 1. Picha<br>2. Manila<br>3. Crayons | |
| (b) Matumizi ya rangi. | Mtoto aweze Kutaja matumizi ya rangi | Kwa kutumia mbinu ya nyimbo, mwalimu awaongoze watoto kutaja matumizi ya rangi. | 1. Picha.<br>2. Vitu halisi.<br>3. Vitu bandia. | 3 |
| (c) Nakshi | Mtoto aweze:-<br>(i) Kuchora mstari wa wima na kulala. | Kwa kutumia mbinu onesho mbinu mwalimu awaongoze watoto kuchora mistari wima na kulala (inayotoka juu kwenda chini na na inayotoka kulia kwenda kusho). | 1. Manila.<br>2. Crayons<br>3. Chati/Chati mguso. | 9 |
| | (ii) Kuunganisha mistari ya wima na kulala | 1. Kwa kutumia mbinu onesho, mwalimu awaongoze watoto kuunganisha mistari ya wima na kulala.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya michezo | 1. Manila.<br>2. Crayons<br>3. Chati/Chati mguso. | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | (games) mwalimu awaongoze watoto kupanga na kupangua vijiti. | | |
| 5. UCHORAJI<br>(a) Maumbo | Mtoto aweze:-<br>(i) Kuainisha sha maumbo. | Kwa kutumia mbinu onesho, mwalimu awaongoze watoto kuainisha majina ya maumbo mbali mbali. Mfano umbo la pembe tatu. . | 1. Chati/Chati mguso<br>2. Kadi.<br>3. Maumbo halisi | 3 |
| | (ii) Kuchora maumbo | Kwa kutumia mbinu onesho, mwalimu awaongoze watoto kuchora na kuonesha wasfu wa maumbo | 1. Mbao<br>2. Vijiti<br>3. Chati/Chati mguso. | |
| (b) Picha | Mtoto aweze:-<br>(I) Kupaka rangi picha | Kwa kutumia mbinu onesho, mwalimu awaongoze watoto kupaka rangi picha | 1. Rangi za maji<br>2. Brashi. | 5 |
| | (ii) Kuchora picha | Kwa kutumia mbinu ya matembezi ukumbini (matembezi ya ndani ya skuli) mwalimu awaongoze watoto kuchora picha walizoziona, | 1. Vitu halisi<br>2. Chati/Chati mguso. | |
| 6. UFUNDI<br>(a) Utungaji | Mtoto aweze:-<br>(i) Kutunga vitu mbali mbali | Kwa kutumia mbinu igizo mfano, mwalimu awaongoze watoto kutunga kwenye vifaa vyenye tundu mfano visoda | 1. Visoda.<br>2. Nyuzi.<br>3. Mshipi. | 6 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | | 4. Mbegu | |
| | (ii) Kushona vitu mbali mbali. | Kwa kutumia mbinu ya igizo mfano mwalimu awaongoze watoto kupitisha uzi kwenye vifaa vyenye tundu (mfano) karatasi | 1. Vijiti<br>2. Karatasi<br>3. Uzi, kitambaa | |
| (b) Ukataji | Mtoto aweze:-<br>Kukata maumbo na picha mbali mbali. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze watoto kukata picha na maumbo mbali mbali. (mfano umbo la mraba, picha ya gari n.k). | 1. Vijiti.<br>2. Picha | 3 |
| (c) Ufinyanzi | Mtoto aweze<br>(i) Kuchanganya udongo. | Kwa kutumia mbinu ya igizo mfano, mwalimu awaongoze watoto namna ya kuchanganya udongo. | 1. Udongo wa ufinyanzi<br>2. Maji. | 6 |
| | (ii) Kutengeneza vitu mbali mbali kwa kutumia udongo. | 1. Kwa kutumia mbinu onesho mbinu mwalimu awaongoze watoto namna ya kutengeneza vitu.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi, mwalimu awaongoze watoto kutengeneza vitu mbali mbali. | 1. Udongo<br>2. Geresho. | |
| (d) Uundaji | Mtoto aweze | Kwa kutumia mbinu ya igizo mfano, | 1. Karatasi | 3 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | Kuunda vitu kwa kutumia vifaa tofauti. | mwalimu awaongoze watoto kuunda vitu tofauti mfano ndege, ngalawa n.k | 2. Vitambaa.<br>3. Manyoya<br>4. Gundi<br>5. Mchanga. | |
| (e) Ususi | Mtoto aweze:-<br>(i) Kusuka | Kwa kutumia mbinu igizo mfano mwalimu, awaongoze watoto kusuka vitu vidogo vidogo mfano mikeka ya karatasi, ukili, mikoba n.k. | 1. Vitambaa.<br>2. Kamba.<br>3. Majani<br>4. Nyuzi.<br>5. Karatasi | 6 |
| | (ii) Kutengeneza vitu | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze watoto kutengeneza vitu mfano vititia, bendera n.k. | 1. Karatasi<br>2. Gundi.<br>3. Vijiti | |
| 6. UCHAPAJI<br>(a) Vifaa | Mtoto aweze:-<br>(i) Kuainisha vifaa vya uchapaji | Kwa kutumia onesho ,mbinu mwalimu awaongoze watoto kutaja na kuonesha vifaa vya uchapaji mfano gurunzi, mbatata, vidaka n.k. | 1. Vidaka.<br>2. Rangi.<br>3. Gurunzi.<br>4. Mbatata n.k. | 2 |
| (b) Kupiga chapa | Mtoto aweze<br>Kupiga chapa kwa kutumia vitu tofauti | Kwa kutumia mbinu onesho mwalimu awaongoze watoto jinsi ya kupiga chapa. | 1. Vidaka.<br>2. Rangi.<br>3. Gurunzi. | 2 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | | 4. Mbatata.<br>5. Majani. | |
| (c) Kukunuta | Mtoto aweze<br>Kukunuta rangi. | Kwa kutumia mbinu ya igizo mfano, mwalimu awaongoze watoto kukunuta rangi kwenye karatasi. | 1. Rangi.<br>2. Brashi.<br>3. Vijiti.<br>4. Karatasi | 2 |
| (d) Kukunja | Mtoto aweze<br>Kupiga chapa | Kwa kutumia mbinu ya igizo mfano, mwalimu awaongoze watoto kupiga chapa mfano kwa kutumia karatasi | . Rangi.<br>2. Brashi.<br>3. Vijiti.<br>4. Karatasi<br>5. Vibao | 3 |

# MWAKA WA PILI

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| 1. HISIA<br>(a) Kuona | Mtoto aweze<br>(i) Kutaja majina ya vitu mbali mbali | Kwa kutumia mbinu ya masuala na majibu mwalimu awaongoze watoto kutaja majina ya vitu vilivyo ndani na nje ya darasa. | Vifaa mfano penseli, meza, mawe, matunda nk. | 3 |
| | (ii) Kuainisha sifa za vitu | Kwa kutumia mbinu ya chemsha bongo mwalimu awaongoze watoto kuainisha vitu kutokana na sifa zake mfano rangi, umbo. | Vifaa mfano penseli, meza, mawe, matunda nk. | |
| (b) Kugusa. | Mtoto aweze Kulinganisha vitu vyenye maumbo na hali mbali mbali. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze watoto kutofautisha na kufananisha vitu vyenye hali na maumbo mbali mbali mfano laini, moto, baridi, vigumu n.k. | 1. Msasa.<br>2. Vibao.<br>3. Sponji<br>4. Soda, juice<br>5. Maji baridi/moto | 2 |
| (c) Kunusa | Mtoto aweze Kuainisha harufu za vitu mbali mbali | Kwa kutumia mbinu onesho mwalimu awaongoze watoto kuonesha na kutaja harufu za vitu walivyovinusa. | 1. Mafuta ya taa.<br>2. Mafuta mazuri.<br>3. Matunda.<br>4. Kitambaa | 2 |
| (d) Kuonja. | Mtoto aweze | Kwa kutumia mbinu ya masuala na majibu | 1. Buni. | 2 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | Kutaja ladha za vitu mbali mbali | mwalimu awaongoze watoto kula vyakula na kunywa vinywaji ili kugundua na kutaja ladha mfano juice, buni, matunda, | 2. Matunda<br>3. Vinywaji. | |
| (e) Kusikia | (i) Kuainisha milio/sauti za vitu mbali mbali. | Kwa kutumia mbinu ya vikundi mwalimu awaongoze watoto kuainisha milio/sauti za vitu walivyosikiliza. | 1. Cherewa.<br>2. CD za sauti za wanyama/ ndege<br>3. Ngoma. | 2 |
| | (ii) Kuigiza milio/sauti walizozisikia. | Kwa kutumia mbinu ya vikundi mwalimu awaongoze watoto kuigiza sauti/milio ya vitu mbali mbali | 1. Cherewa.<br>2. CD za sauti za wanyama/ ndege<br>3. Ngoma. | |
| 2. MAIGIZO<br>(a) Udhibiti wa sauti katika uigizaji | Mtoto aweze:-<br>Kutoa sauti kulingana na kitendo anachoigiza. | Kwa kutumia mbinu igizo mwalimu awaongoze watoto<br>kutoa sauti kulingana na kitendo anachoigiza katika maigizo yao. | 1. Vitu halisi.<br>2. Vitu bandia.<br>3. CD. | 3 |
| (b) Udhibiti wa sauti katika uimbaji | Mtoto aweze:-<br>(i) Kupandisha na kushusha sauti kulingana na | Kwa kutumia mbinu ya nyimbo mwalimu awaongoze watoto kuimba nyimbo fupi zenye maadili zinazoonesha kupandisha na kushusha kwa sauti. | 1. CD.<br>2. Kanda za redio. | 3 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | wimbo unaoendana na tukio. | | | |
| (c) Michezo midogo midogo. | Mtoto aweze Kuigiza michezo tofauti. | Kwa kutumia mbinu ya vikundi mwalimu awaongoze watoto kuigiza michezo midogo midogo yenye maadili katika nafasi tofauti itakayowashirikisha watoto wengi. | 1. CD.<br>2. Kanda za redio.<br>3. Vitu halisi.<br>4. Vitu bandia | 6 |
| 3. UIMBAJI<br>(a) Matumizi ya sauti katika nyimbo, kasida. | Mtoto aweze:-<br>(i) Kueleza hisia zao kwa kuimba nyimbo. | Kwa kutumia mbinu ya nyimbo mwalimu awaongoze watoto kuimba nyimbo za kielimu wanazozifahamu. | 1. CD.<br>2. Kanda za redio<br>3. Redio. | 4 |
| | (ii) Kusoma kasida. | Kwa kutumia mbinu ya nyimbo mwalimu awaongoze watoto kusoma kasida za kielimu wanazozifahamu. | 1. CD.<br>2. Kanda za redio.<br>3. Redio | |
| | (iii) Kutofautisha sauti ya nyimbo na kasida kwa | Kwa kutumia mbinu ya nyimbo mwalimu awaongoze watoto kutofautisha sauti ya nyimbo na kasida kwa kuzingatia mapigo | 1. CD.<br>2. Kanda za redio. | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | kuzingatia mapigo. | ya uimbaji. | 3. Redio.<br>4. Ala za muziki. | |
| 4. UCHORAJI<br>(a) Ubunifu wa picha kutokana na maumbo. | Mtoto aweze<br>Kubuni picha mbali mbali kutokana na maumbo. | Kwa kutumia mbinu onesho mwalimu awaongoze watoto kubuni picha za vitu tofauti kutokana na maumbo, | 1. Maumbo.<br>2. Vibao.<br>3. Rangi.<br>4. Maboksi.<br>5. Chati/Chati mguso. | 3 |
| (b) Uchoraji wa kujieleza. | Mtoto aweze<br>Kuchora picha kutokana na hadithi na vitendawili. | Kwa kutumia mbinu ya kusimuliana hadithi mwalimu awaongoze watoto kuchora picha kutokana na hadithi na vitendawili. | 1. Vitabu vya hadithi.<br>2. Rangi.<br>3. Karatasi. | 6 |
| (c) Nakshi. | Kuchora nakshi na mapambo yake. | Kwa kutumia igizo mfano mwalimu awaongoze watoto kuchora picha zinazotokana na nakshi.mfano nakshi ya misumeno, kitumbo juu n.k. | 1. Chati<br>2. Vitu halisi. | 6 |
| (d) Maumbo | Mtoto aweze:-<br>Kuunganisha maumbo kwa kupata picha mbali mbali. | Kwa kutumia mbinu ya kucheza (games) mwalimu awaongoze watoto kuunganisha maumbo kwa kupata picha mbali mbali. | 1. Vibao.<br>2. Manila.<br>3. Rangi.<br>4. Maumbo. | 4 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| 5. UFUNDI<br>(a) Utungaji | Mtoto aweze:-<br>(i) Kutunga vitu mbali mbali. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze watoto kutunga vifaa vyenye tundu mfano visoda. | 1. Visoda.<br>2. Nyuzi.<br>3. Mishipi.<br>4. Mbegu. | 6 |
| | (ii) Kushona vitu mbali mbali. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze watoto kupitisha uzi kwenye vifaa vyenye tundu mfano karatasi. | 1. Vijiti.<br>2. Karatasi.<br>3. Uzi.<br>4. Vitambaa<br>5. Viatu (buti). | |
| (b) Ukataji | Mtoto aweze<br>Kukata maumbo na picha | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze watoto kukata picha na maumbo tofauti mfano umbo la mstatili picha ya nyumba n.k. | 1. Mkasi.<br>2. Picha.<br>3. Boksi.<br>4. Manila.<br>5. Vitambaa. | 3 |
| (c) Ufinyanzi. | Mtoto aweze<br>Kubuni na kufinyanga vitu tofauti. | 1. kwa kutumia mbinu ya igizo mfano mwalimu awaongoze watoto namna ya kuchanganya udongo.<br>2. Kwa kutumia mbinu onesho mwalimu awaongoze watoto namna ya kutengeneza vitu vya udongo. | 1. Udongo wa ufinyanzi.<br>2. Maji.<br>3. Modeli za vitu. | 5 |
| (d) Ubunifu | Mtoto aweze | Kwa kutumia mbinu ya igizo mfano | 1. Maboksi. | 5 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | Kutumia vifaa mbali mbali kwa kukata,kuchana na kubandika.(collage) | mwalimu awaongoze watoto kukata, kuchana na kubandika ili kutengeneza vitu kwa kutumia vifaa viliopo. | 2. Gundi.<br>3. Vitambaa.<br>4. Mchanga | |
| (e) Ususi. | Mtoto aweze<br>(i) Kusuka. | Kwa kutumia mbinu igizo mfano mwalimu awaongoze watoto kusuka vitu vidogo vidogo mfano mikeka ya karatasi, mikoba n.k. | 1. Manila.<br>2. Vitambaa.<br>3. Kamba.<br>4. Ukili.<br>5. Makuti.<br>6. Nyuzi n.k. | 6 |
| | (ii) Kutengeneza vitu. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze watoto kutengeneza vitu tofauti mfano vititia, bendera n.k. | 1. Karatasi.<br>2. Gundi.<br>3. Makuti. | |
| 6. UCHAPAJI<br>(a) Kupiga chapa | Mtoto aweze:<br>(i) Kupiga chapa kwa kutumia vifaa tofauti. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze watoto kupiga chapa vitu tofauti. | 1. Mbatata.<br>2. Vidaka.<br>3. Rangi za maji. | 6 |
| | (ii) Kubuni vitu mbali mbali. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze watoto kubuni vitu tofauti mfano kanga , vitambaa n.k. | 1. Mbatata.<br>2. Vidaka.<br>3. Rangi za maji | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| (b) Kukunuta | Mtoto aweze Kukunuta rangi. | Kwa kutumia mbinu ya igizo mfano mwalimu awaongoze watoto kukunuta rangi kwenye karatasi. | 1. Rangi.<br>2. Brashi.<br>3. Vijiti. | 3 |
| (c) Kukunja | Mtoto aweze Kupiga chapa kwa kukunja karatasi. | Kwa kutumia mbinu ya igizo mfano mwalimu awaongoze watoto kupiga chapa kwenye karatasi na kukunja.. | 1. Rangi.<br>2. Brash.<br>3. Vijiti.<br>4. Karatasi. | 4 |